**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

SHULE YA SEKONDARI UKWIVA,
S.L.P 344,
KILOSA.

07/12/2020.

**KUMB.NA.EF/USS/SA/VOL.II/13**
KWA.......................................................................
.............................................................................
.............................................................................

## UTARATIBU WA KUJIUNGA NA SHULE

Napenda kukujulisha kwamba umechaguliwa kujiunga na shule ya Sekondari UKWIVA kidato cha kwanza mwaka 2021. **HONGERA SANA.**

Shule ya Sekondari **UKWIVA** ipo katika kata ya Ulaya, katika eneo la Ulaya Mbuyuni jirani kabisa na Shule ya msingi Ulaya Mbuyuni, barabara ya Kilosa-Mikumi.

Shule ni ya kutwa haina HOSTEL, hivyo jukumu la kujitafutia malazi ni lako mwenyewe.

Ni vyema ukiwa na baiskeli kurahisisha usafiri wa kuwahi shule wakati wa asubuhi. Shule haiwajibiki kulipa gharama za usafiri wala matibabu ya mwanafunzi. Ipo zahanati ya Kata hiyo inayotoa matibabu karibu na Shule. Inashauriwa kwa wanafunzi wanaotoka nje ya kata ya Ulaya na kuja kuishi nyumba za kupanga jirani na shule kuwafungulia wanafunzi hao bima ya afya au kumpatia fedha ili kusaidia matibabu pindi mwanafunzi anapougua akiwa shuleni.

Masomo yataanza tarehe 11/01/2021 wanafunzi wanapaswa kufika shuleni tarehe 11/01/2021 kwa usajili na kuanza kozi maalumu ya Kiingereza.

### SEHEMU A: NYARAKA MUHIMU ZA KUJA NAZO

1: **HATI YA URAIA**
Cheti cha kuzaliwa

2: **UTHIBITISHO WA AFYA**

Peleka fomu iliyoambatishwa kwa Mganga Mkuu wa Wilaya yako ili upwimwe afya yako. Upimaji ufanyike katika Hospitali ya Wilaya au Kituo cha Afya.

3: Fomu ya kukubali Sheria na masharti ya Shule.

Fomu iliyoambatishwa kwenye barua hii ijazwe kikamilifu na mwanafunzi na mzazi/mlezi na kuwasilishwa shuleni siku ya kufungua Shule.

Scanned with CamScanner

## SEHEMU B: SARE YA SHULE.

### 1: WAVULANA

(A) Sare wakati wa masomo

- (i) Mashati mawili meupe ya mikono mifupi.
- (ii) Suruali mbili rangi ya Ugoro, zenye marinda mawili( 2).
- (iii) Mkanda wa suruali mweusi au kahawia-usiokuwa na marembo yoyote
- (iv) Viatu vya ngozi nyeusi vya kamba na visigino vifupi si zaidi ya nchi moja.
- (v) Soksi nyeusi (Jozi mbili).
- (vi) Raba za michezo rangi nyeusi.
- (vii) Sweta ya rangi ya ugoro.

### 2: WASICHANA.

(B) Sare wakati wa masomo

- (i) Mashati mawili meupe ya mikono mifupi.
- (ii) Sketi mbili rangi ya ugoro ndefu ( inch 8/cm 20) kutoka chini kwenye nyayo.
- (iii) Viatu vyeusi vya ngozi nyeusi vyenye kamba visiwe na kisigino kirefu, kisizidi inchi moja.
- (iv) Soksi nyeupe ndefu zisizo na urembo wowote.
- (v) Sweta rangi ya ugoro.
- (vi) Mshono wa sketi rinda box yenye marinda matatu( 3) kila upande na belti iwe na upana wa inchi mbili( 2).

**NB**: (i) Ili kudhibiti aina ya kitambaa na rangi Shule imeandaa kitambaa cha mfano ambacho kimeambatishwa na fomu hii/ambacho kitapatikana eneo litakaloelekezwa.

(ii) Mwanafunzi aje na picha nne passport size(ziwe na back ground ya bluu) akiwa amevaa sare ya Shule.

**VIFAA VYA USAFI**

- (i) Kila mwanafunzi aje na jembe.
- (ii) Wavulana waje na panga jipya.
- (iii) Wasichana waje na fyekeo jipya.
- (iv) Wote waje na mafagio ya chelewa.

## SEHEMU C: VIFAA VYA MASOMO

Mwanafunzi anatakiwa kuja na

- i. Mdaftari makubwa (counter books) kumi.
- ii. Kalamu ya wino na risasi au penseli.
- iii. Mkoba wa kubebea madaftari ( school bag).
- iv. Mkebe wa vifaa vya Hisabati.(Mathematical set).
- v. Dictionary (Kamusi) English-English.

## SEHEMU: D

Shule inatoa chakula cha mchana kwa wanafunzi wote hivyo ni jukumu la mzazi kuchangia chakula hicho kama ifuatavyo.(maelezo zaidi yatapatikana shuleni siku ya kuripoti mwanafunzi).

- Mahindi debe moja( 1) kwa kila muhula.
- Maharage sado moja (01) kwa kila muhula, kipimo ni sado (Lt.5).
- Fedha T.Shs. 8000/= kwa kila muhula kwa ajili ya kusaga na kukoboa , kununua viungo na kulipa mpishi nk.

Scanned with CamScanner

NB: Wanafunzi wote waje na chakula hicho cha muhula wa kwanza anapokuja kuripoti shuleni tarehe 11/01/2021.

**MUHIMU SANA**

Ndugu mzazi, mlezi tafadhali hakikisha unamleta mwanao akiwa amevaa sare kamili ya shule kuepuka usumbufu usiokuwa na sababu unaoweza kujitokeza.

.......................................

**IPYANA D. KILASILE**
**MKUU WA SHULE**
**0757912846**

THE HEADMASTER
UKWIVA SECONDARY SCHOOL
P.O. BOX 304 KILOSA

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALIMASHAURI YA WILAYA YA KILOSA**
**SHULE YA SEKONDARI UKWIVA**

## SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

1. Wanafunzi wanatakiwa kusimama na kumsalimu mwalimu au mtu yeyote anayewazidi umri.

2. Wanafunzi hawaruhusiwi kutumia lugha mbaya wakati wowote kati yao wenyewe, kwa walimu wao na kwa watu wengine.

3. Wanafunzi wanatakiwa kuitika mara moja na kukimbilia aliko Mkuu anayewaita.

4. Wanafunzi wanatakiwa kuhudhuria vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa.

5. Wanafunzi wanatakiwa kukaa kimya darasani na wasitoke bila ruhusa ya Mwalimu au kiongozi aliyeko.

6. Wanafunzi wahudhurie mikutano ya shule , mfano Baraza, Ukaguzi wa Usafi, Kupandishwa bendera ya Taifa n.k.

7. Wanafunzi wanatakiwa kuheshimu baraza, mikutano, Ofisi za Shule mali binafsi na mali ya umma.

8. Wanafunzi wanatakiwa kufuata ratiba ya kila siku kama ilivyopangwa.

9. Wanafunzi wanaposikia wito wa dharura wawahi.

10. Wanafunzi wanatakiwa kuvaa sare ya Shule muda wote wa
    **a)** Masomo ya darasani
    **b)** Wanapotoka nje ya Shule kwa shughuli za Shule
    **c)** Mhadhara/ baraza la Shule
    **d)** Maandamano

11. Wanafunzi hawaruhusiwi kuvaa sare ya Shule na ;
    a) Kofia
    b) Viatu vya ghorofa
    c) Mapambo mengineyo

12. Wanafunzi wanatakiwa kuwa wasafi wa mavazi yao na mazingira kwa ujumla.

13. Wanafunzi wasitoke nje ya mipaka ya Shule isipokuwa kwa kibali maalumu.

14. Wanafunzi hawaruhusiwi kufanya mambo yafuatayo:

Scanned with CamScanner

a) Kuvuta sigara au ugoro.
b) Kufuga kucha ndefu.
c) Kuwa na nywele ndefu.
d) Kunyoa mitindo ya kihuni au kipara.
e) Kutumia vinywaji vya kulevya au madawa ya kulevya.
f) Kuvaa mavazi yasiyo na heshima.
g) Kugombana na kupigana.
h) Kufika shuleni na simu au Redio.

15. Wanafunzi wasitembelee sehemu zifuatazo;
   a) Vilabu vya pombe.
   b) Majumba ya starehe.
   c) Nyumba za wageni.

16. Wanafunzi wasitembelee sehemu zifuatazo isipokuwa kwa kibali maalum
   a) Chumba cha Walimu.
   b) Ofisi za shule.
   c) Maabara.
   d) Nyumba za Walimu na wafanyakazi wasio walimu.

17. Mzazi/Mlezi atamwombea mwanae ruhusa wakati wa masomo kwa **Maandishi** na wala siyo kwa **Simu.**

18. Mwanafunzi asipohudhuria masomo kwa siku 3 bila taarifa hatapokelewa mpaka mzazi/mlezi afike Shuleni.

19. Makosa yafuatayo yanaweza kukusababisha kufukuzwa Shuleni mara moja;
   a) Wizi.
   b) Uasherati, Ubakaji, Ushoga na Usagaji na Madawa ya kulevya.
   c) Ulevi.
   d) Uvutaji bangi.
   e) Makosa ya jinai.
   f) Kupigana au kupiga.
   g) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
   h) Kuoa au kuolewa.
   i) Kupata mimba au kusababisha mimba ndani au nje ya Shule.
   j) Kutoa mimba.
   k) Kugoma, kuchochea au kuongoza mgomo, au kuvuruga amani au usalama wa watu.
   l) Kukataa adhabu halali kwa makusudi.

……………………………………

**MKUU WA SHULE**

THE HEADMASTER
UKWIVA SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 344 KILOSA

Scanned with CamScanner

**THE PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**KILOSA DISTRICT COUNCIL**

UKWIVA SECONDARY SCHOOL,
P.O.Box 344,
**KILOSA.**

**REF. No. USS/REG/VOL.1/..........** ..................

**<u>REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.</u>**

FROM: THE MEDICAL OFFICER
GOVERNMENT HOSPITAL
.......................................
.......................................

TO: THE HEAD OF SCHOOL,
UKWIVA SECONDARY SCHOOL,
P.O.Box 344,
**KILOSA.**

**RE: MEDICAL CERTIFICATE FORM.**

I have examined ............................................................... who aspires to join form one in your school as follows:-

| No | AREA | REMARKS |
|---|---|---|
| 1 | Skin | |
| 2 | Eyes | |
| 3 | Ears | |
| 4 | Teeth | |
| 5 | Chest | |
| 6 | Spleen | |
| 7 | Abdomen | |
| 8 | Urine | |
| 9 | Stool | |
| 10 | HB Hemoglobin | |
| 11 | In a collation against meningitis | |
| 12 | Sickle cells | |
| 13 | Asthma | |
| 14 | Pregnancy (If applicable) | |

ADDITION INFORMATION:- Eg. Physical defects or impairments, infection, chronic or family diseases etc.
.............................................................................................
.............................................................................................
.............................................................................................

I certify that the above is physical fit/unfit for admission
Signature ................................................
Destination ..............................................
Station ....................................................
Date .........................................................
Official Stamp ..........................................

Scanned with CamScanner

# OFISI YA RAIS
## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
## HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOSA
## SHULE YA SEKONDARI UKWIVA
## S.L.P. 344, KILOSA

---

**FOMU YA TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI NA KUKUBALI SHERIA NA NAFASI YA SHULE ALIYOPEWA.**

**A: TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI:**

- JINA LA MWANAFUNZI (Taja majina matatu)
  ...................................................................................................
- TAREHE YA KUZALIWA: .....................................................................
- MAHALI ALIPOZALIWA (MKOA/WILAYA) ..............................
- MNAISHI/MNAKAA WAPI? ..................................................
  KATA/MTAA .............................................
- URAIA: .........................................................................................
- SHULE ALIYOTOKA: ...................................................................
- NAMBA YA MTIHANI (PSEE) ...............................................

**TAARIFA YA MZAZI/MLEZI:**

- JINA LA MZAZI/MLEZI (Taja majina matatu)
  ...................................................................................................
- KAZI YA MZAZI/MLEZI: ......................................................
- ANUANI YA MZAZI/MLEZI: ...................................................
- SIMU YA MZAZI/MLEZI: .......................................................

**KUKUBALI NAFASI NA MAELEKEZO ULIYOPEWA**

Mimi ..................................................kidato: .................. Mwaka ........... Nimesoma na kuyaelewa maelekezo yote, kwa hiyo nakubali kuipokea/sikubali kuipokea nafasi niliyopewa. Nathibitisha kwamba nimepokea maagizo/maelekezo na bila kulazimishwa naahidi kuyazingatia.
Tarehe: ......................... saini: ...........................

**KUKUBALI SHERIA ZA SHULE:**
**MWANAFUNZI**
Mimi .................................................... nimezisoma na kuzielewa sheria za shule na ninaahidi nitazingatia na kutii masharti, sheria za shule na maelekezo mengine nitakayopewa na Walimu na viongozi wote wa shule, nikikiuka sheria hizo hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi yangu kwa mujibu wa kanuni, taratibu na sheria zilizopo.
Tarehe ............................................... Saini ...........................................

**MZAZI/MLEZI (Ajaze sehemu hii)**
Mimi Mzazi/Mlezi wake nathibitisha kuwa mwanangu ................................ ameelewa maagizo na ninapenda ifahamike kuwa dini ya mwanangu ni ................................ madhehebu/dhehebu lake ni ..................................

Aidha, mimi ................................................ ambaye ni mzazi/mlezi, nimesoma/nimesomewa sheria na maagizo mengine ya shule yanayomhusu mwanafunzi ...................................... Na ninaahidi kutimiza wajibu wangu nikiwa mzazi/mlezi wa mtoto huyu kwa kumshauri ipasavyo pamoja na kumtimizia mahitaji yake ya shule.

| | |
|---|---|
| ............................................... | ................................... |
| JINA LA MZAZI/MLEZI | SAINI YA MZAZI/MLEZI |

..........................
TAREHE

Scanned with CamScanner